# Maswali Yanayoulizwa Sana Kuhusu Ufikiaji wa Vyakula

Katika nyakati hizi ngumu, kuna maswali mengi kuhusiana na upatikanaji wa chakula, kutoka miongoni mwa watu ambao hutegemea mipango mahususi ya huduma za kibinadamu, na wale ambao ni watumiaji wa kwanza wa manufaa ya umma.

**Je, ni mipango gani ya umma ya manufaa ya chakula inayopatikana?**

Kuna aina nyingi za mipango zinazopatikana na ustahiki kwa mipango hiyo hutofautiana, kama vile chakula cha mchana cha "kuchukua na kuondoka kwa haraka" kwa wanafunzi na mipango ya milo inayopelekwa nyumbani kwa watu wazee au watu walio na ulemavu. Mpango unaojulikana zaidi ni Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada.

**Je, mahitaji ya ustahiki ni yapi kwa SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada)?**

SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada) ni mpango ambao ustahiki wake unategemea mapato. Miongozo kamili na orodha ya mapato inaweza kupatikana katika tovuti ya Idara ya Huduma za Binadamu ya PA.

**Je, naweza vipi kutuma maombi ya SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada)?**

Watu binafsi na familia wanaweza kujaza maombi ya SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada) mtandaoni kupitia mfumo wa manufaa ya COMPASS au uchapishe nakala kutoka kwa tovuti kisha uitume kwa barua. Greater Pittsburgh Community Food Bank (Hifadhi ya Chakula cha Jamii ya Greater Pittsburgh) na Just Harvest zote zinatoa usaidizi katika kujaza maombi. Mara ombi linapoidhinishwa, utapokea kadi ya malipo ya SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada).

**Je, ninaweza kutumia kadi yangu ya SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada) mtandaoni?**

Kadi za SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada) kwa sasa haziwezi kutumika kwa malipo ya mtandaoni. Ingawa agizo la vyakula linaweza kufanywa mtandaoni (ikiwa duka fulani linatoa chaguo hilo), kadi ya SNAP (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada) lazima iwasilishwe kwenye eneo la duka na mtu anayeaminika ambaye ana PIN sahihi.

**Je, ninaweza kupata wapi chakula?**

Unaweza kupiga simu wakati wote kwa 2-1-1 (http://pa211sw.org) au wasiliana na Greater Pittsburgh Community Food Bank (Hifadhi ya Chakula cha Jamii ya Greater Pittsburgh) (www.pittsburghfoodbank.org) kwa ajili ya msaada wa kupata machaguo ya chakula ambayo yanashabihiana na mahitaji yako. Ramani ya maeneo ya chakula, inayopatikana hapa, inayodumishwa kwa ushirikiano na Hifadhi ya Chakula cha Jamii ya hutoa orodha iliyosasishwa ya mikahawa ya vyakula na chaguo zingine za chakula cha dharura kote katika kaunti. Ramani hiyo inaweza kupatikana kwa mahitaji mahususi ya chakula (kama vile milo ya shule ya "kuchukua na kuondoka haraka" au milo kwa watu wazee) na inaorodhesha anwani za tovuti, saa za kazi na maelezo ya mawasiliano ikiwa yanapatikana.

Hifadhi ya Chakula cha Jamii inatekeleza usambazaji wa chakula katika nyakati na maeneo mahususi kote katika kaunti. Kwa kawaida matukio haya huwa makubwa na huhitaji muda mrefu wa kusubiri, na yanafaa kwa familia zisizo na chaguo zingine. Nyakati na maeneo ya usambazaji yanapatikana kwenye tovuti ya hifadhi ya chakula.

**Je, ninaweza kupata wapi fomyula ya maziwa ya mtoto?**

Ramani ya maeneo ya chakula inajumuisha maeneo ya Vituo vya Familia kote katika kaunti ambayo yana uwezo wa kutoa fomyula za maziwa ya mtoto kwa kuchukua na kuondoka haraka kwa familia. Tafadhali tumia maelezo ya mawasiliano kwenye ramani ili upige simu kabla ili kupanga jinsi ya kuchukua, kwani maeneo haya hayapo wazi kwa umma.

**Vipi kama siwezi kutoka nyumbani kwenda kununua chakula?**

Rafiki yako au jamaa anaweza kukuchukulia chakula, lakini tovuti nyingi zina miongozo ya nyaraka zipi wanahitaji wanaokuchukulia chakula wazionyeshe. Tumia maelezo ya mawasiliano kwenye ramani ya maeneo ya chakula ili upige simu kabla ili ujue eneo ulilochagua linahitaji nini kutoka kwako.

Ikiwa hakuna mtu anayeweza kukuchukulia chakula, kuna baadhi ya vikundi vya jamii ambavyo hutoa huduma za kupeleka chakula nyumbani. Piga simu 2-1-1 (au utembelee http://pa211sw.org) au usiliane na Hifadhi ya Chakula (www.pittsburghfoodbank.org) ili ufahamu chaguo zinazopatikana za kuletewa chakula nyumbani.

**Je, Mpango wa Home Delivered Meals (HDM) (Kupeleka Chakula Nyumbani) kwa Watu Wazee wa Shirika la Eneo bado unafanya kazi?**

Ndiyo, mpango wa HDM (Kupeleka Chakula Nyumbani) unafanya kazi kikamilifu na rufaa mpya kwa HDM (Kupeleka Chakula Nyumbani) zinawasilishwa kupitia Allegheny County Department of Human Services Area Agency on Aging SeniorLine (Shirika la Eneo la Idara ya Huduma za Binadamu ya Kaunti ya Allegheny katika Mfumo wa Mawasiliano ya Watu Wazee) kupitia 412-350-5460. Kwa sasa, Mpango wa Milo ya Kupelekwa Nyumbani unawasilisha milo iliyogandishwa. Siku za uwasilishaji wa milo hiyo hutofautiana kulingana na Mtoa huduma.

**Je, Vituo vya Huduma kwa Watu Wazee vinaendelea kutoa chakula?**

Ndiyo, vituo vyote vya huduma kwa watu wazee vinatoa milo ya "kuchukua na kuondoka haraka" kwa washiriki wa kawaida wa chakula kutoka kituo cha huduma kwa watu wazee ambao wanahitaji chakula. Wasiliana na kituo chako ili kujua mchakato wa jinsi ya kuchukua chakula. Ikiwa haujasajiliwa katika kituo cha huduma kwa watu wazee na una umri wa zaidi ya 60, piga simu kwa Allegheny County Department of Human Services Area Agency on Aging SeniorLine (Shirika la Eneo la Idara ya Huduma za Binadamu ya Kaunti ya Allegheny katika Mfumo wa Mawasiliano ya Watu Wazee) kupitia 412-350-5460 kwa maelezo na usaidizi.

**Je, ni usaidizi gani mwingine unaopatikana?**

The Coronavirus Aid, Relief and Economic Security (CARES) Act (Sheria ya Msaada wa Virusi vya Korona, Unafuu na Usalama wa Kifedha) iliyotiwa saini hivi karibuni ilijumuisha uanzishaji wa manufaa ya Pandemic Unemployment Assistance (PUA) (Usaidizi kwa Wasio na Ajira Kutokana na Janga). Maelezo ya ustahiki wa PUA (Usaidizi kwa Wasio na Ajira Kutokana na Janga) yanaweza kupatikana hapa. Orodha ya raslimali na haki za ukosefu wa ajira kwa Pennsylvania inaweza kupatikana katika https://www.attorneygeneral.gov/covid-rights. Ikiwa unahitaji nepi au bidhaa za usafi (bidhaa ambazo hazitolewi na SNAP) (Mpango wa Usaidizi wa Lishe ya Ziada), maeneo ya kupata bidhaa hizi yanatambuliwa kwenye ramani ya maeneo ya chakula.